JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MOMBA

Simu: 0272970056
S.L.P 273,
Momba, Songwe

Barua pepe: ded@mombadc.go.tz
Tovuti: http:www.mombadc.ac.tz

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI KWA FUNDI MKUU UJENZI (LOCAL TECHNICIAN IN BUILDING WORKS) UJENZI WA NYUMBA YA WAGENI (REST HOUSE)

TAREHE: 20/09/2022

ZABUNI NAMBA:LGA/142/2022-2023/W/01

Kwa kusudi la kuboresha mapato ya ndani, Halmashauri ya Wilaya ya Momba, inatarajia kujenga Nyumba ya kulala Wageni (Rest House), Makao makuu ya Halmashauri kijiji cha Tindingoma.

Mradi huu unatekelezwa kwa mwongozo wa **'FORCE ACCOUNT'** kama ilivyoelekezwa na Serikali kupitia miongozo mbalimbali na kusimamiwa na Wataalamu wa ndani ya Halmashauri.

Hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kupitia kamati ya mradi wa Ujenzi, anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi tajwa hapo juu katika fani, sifa na masharti kama yaliyoainishwa katika tangazo hili kuomba kazi:

## A) FANI NA MASHARTI/SIFA MAHUSUSI ZA FUNDI MKUU ZINAZOHITAJIKA;

### SIFA ZA FUNDI MKUU UJENZI:

1) Kwa kuzingatia ukubwa wa kazi hii Fundi mkuu lazima awe Mhandisi wa ujenzi *(Civil and or related Civil Engineering)*, au Fundi Sanifu Ujenzi (FTC/Diploma) Msanifu majengo *(Architect)* au Mkadiria majenzi *(Quantity Surveyor)* mwenye uzoefu wa miaka angalau mitano. Fundi mkuu Lazima aambatanishe cheti cha shahada au FTC/Diploma, mikataba na hati za malipo kwa kazi alizowahi kufanya pamoja na 'CV' yake.
2) Fundi mkuu lazima awe na mafundi wasaidizi angalau watatu (03) kwa kila fani tajwa hapo juu (Uashi, Kupaua na Rangi) na aambatanishe nyaraka za mafundi hao zikionesha uzoefu wa kazi walizofanya.
3) Kwa kuwa hakutakuwa na malipo ya awali kwa fundi mkuu na kwa kuzingatia ukubwa wa kazi hii, lazima fundi mkuu awe na mtaji ili kuwalipa mafundi wake wasaidizi na awasilishe pamoja na nyaraka zake nakala ya *'bank statement' ya angalau miezi sita (06) nyuma ya tarehe ya tangazo hili* ili kuthibitisha mtaji alionao wa kuwalipa mafundi wake wasaidizi na vibarua watakao fanya kazi hii.
4) Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na hii kwa mwongozo wa *'Force Account'* na Lazima aambatanishe nyaraka zifuatazo ili kuthibitisha kuwa ni kweli amewahi kufanya na kukamilisha bila shaka:
   a) Mkataba wa kazi inayofanana na hii
   b) Hati za malipo ya gharama za ufundi (payment certificate).

c) 'Bank Statement' ikionesha gharama za malipo ya ufundi aliyolipwa yenye thamani za kazi alizofanya katika kipindi tofauti tofauti.

Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kupaua paa za aina mbalimbali katika majengo ya serikali.

5) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kupaua mabati ya aina zote na kufanya '*brandering & ceiling*

6) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kutumia mitambo na vifaa mbalimbali vya ujenzi

7) Fundi lazima aandae na kuwasilisha mpango kazi ukielezea shughuli na muda wa utekelezaji wa mradi sambamba na nyaraka nyingine katika tangazo hili.

8) Fundi mkuu lazima awasilishe bahasha moja ambayo itakuwa na nyaraka tajwa katika tangazo hili ikiwa pamoja na gharama za ufundi.

9) Nakala ya Michoro na fomu za mchanganuo wa shughuli za ujenzi za mradi huu zinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Halmashauri ya Wilaya Momba .

10) Fundi lazima aombe na kujaza kazi zote (Uashi, Kupaua, Rangi) kama ilivyooneshwa katika tangazo hili. Fundi ambaye ataacha kujaza kipengele kimojawapo miongoni mwa vipengele tajwa hapo juu maombi yake hayatafanyiwa kazi.

11) Inasisitizwa kuwa fundi mkuu anatakiwa kujaza gharama za ufundi tuu (Labour Charges) kwa kazi tajwa na kusudiwa kwa mujibu wa tangazo hili.

## B) MASHARTI YA UJUMLA KWA MWOMBAJI;

1) Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18.
2) Mwombaji lazima awe na Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN).
3) Mwombaji lazima awe na Akaunti ya benki iliyo hai.
4) Mwombaji lazima aandike barua ya maombi kwa jina lake na siyo Kampuni au jina la biashara.
5) Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya 'ki-eletroniki'na posta hayatapokelewa.
6) Mwombaji lazima aambatanishe barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Kijiji/mtaa.
7) Barua za maombi ziwasilishwe kwa njia ya mkono ofisi za masijala (Registry Office) za Halmashauri ya Wilaya ya Momba, zikiwa zimeandikwa juu ya bahasha kwa herufi kubwa:

   KATIBU, BODI YA ZABUNI
   HALMASHAURI YA WILAYA MOMBA,
   MRADI WA UJENZI WA NYUMBA YA KULALA WAGENI (REST HOUSE),
   S. L .P, 273, MOMBA
8) *Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe 27/09/2022 saa 11:30 Asubuhi na ndiyo siku ya ufunguzi wa bahasha za maombi na usahili wa mafundi kwa kazi hii.*
9) Kwa maelezo zaidi wasiliana kwa namba +255757 685 284 AU +255762 512 104) Siku ya kutembelea na kuona eneo la ujenzi 27/09/2022 saa 08:00 Mchana.

Tangazo hili Limetolewa na:

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
P.O BOX 273
TUNDUMA MOMBA
MOMBA DISTRICT COUNCIL

..............................................

REGINA L. BIEDA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MOMBA